**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA**

**Simu:** +2552737928765/0783334545, **Barua pepe:**prungemba@jamii.go.tz,
**Tovuti:** www.rungembacdti.ac.tz S.L.P 6, Mafinga

**Kumb. Na. CD/C/2/10/48** **08/06/2026**

**Ndugu**

..............................................

..............................................

..............................................

**YAH: TAARIFA YA KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA CHETI YA MAENDELEO YA JAMII NA UPANGAJI NA USIMAMIZI WA MIRADI (BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN COMMUNITY DEVELOPMENT& PROJECT PLANNING AND MANAGEMENT) MWAKA WA MASOMO 2026/2027**

***CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA NI CHUO CHA JINSI YA KIKE TU.***

1. Uongozi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba unayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba katika mwaka wa masomo 2026/2027 kwa mafunzo ya ngazi ya Astashahada (**Basic Technician Certificate in Community Development & Project planning Management- NTA LEVEL 4**).
2. **Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba** kipo kata ya Rungemba, Halmashauri ya Mji Mafinga, Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa ambapo ni takribani kilomita 65 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, barabara kuu ya kuelekea Mbeya na km 15 kutoka Mafinga mjini kuelekea Iringa. Mwanachuo atashuka kituo cha mabasi kiitwacho **Makwawa.**
3. Chuo kitafunguliwa tarehe **1 9 /10/2026,** unatakiwa chuoni tarehe tajwa.
   Mara ufikapo chuoni utapewa kanuni na taratibu za chuo na utapata fursa ya kujizoeza mazingira ya chuo (Orientation), zoezi hilo litafanyika kati ya tarehe 26-29/11/2026. Aidha utatakiwa kushiriki kikamilifu katika mafunzo ya nadharia darasani na vitendo uwapo chuoni. Mwanachuo uje na vitu vifuatavyo:-
   i. Ream Paper moja (1) **nyeupe A4 NO.1**
   ii. Nakala (copy) ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne au results slip kama cheti cha kidato cha nne hakijatoka
   iii. Nakala (copy) ya cheti cha kuzaliwa
   iv. Picha tatu **(Passport size blue coloured**) zilizopigwa ndani ya miezi sita
   v. Blanket mbili, Shuka mbili, Mto wa kulalia, Ndoo, na Chandarua kwa matumizi yako, **kitanda na godoro vinapatikana chuoni**

4. Gharama za usafiri kuja chuoni na kurudi nyumbani wakati wote ni jukumu lako/mzazi/mlezi.
5. Chakula kinatolewa na mzabuni kwenye Kantini ya chuo. Mwanafunzi atalazimika kula

kwenye kantini za chuo na si vinginevyo. **Fedha kwa ajili ya chakula zitagharamiwa na mzazi au mlezi wa mwanachuo,** makadirio ya fedha ya chakula angalia kipengele namba **C: POCKET MONEY.** Mwanachuo haruhusiwi kupika au kuchemsha maji katika majengo yoyote ya chuo.

6. Kwa sasa chuo kina nafasi za kutosha za bweni. Hivyo wanafunzi wote wanalazimika kukaa hosteli kwa ajili ya kulinda maadili yao pamoja na wasifu wa chuo

7. Mwanachuo hataruhusiwa kuwa na vifaa vya umeme ndani ya bweni kama vile pasi, heater, TV, jiko, blender n.k. Kuna sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili ya kunyosha nguo.
8. Chuo hakina sare kwa sasa, ila Mavazi ya heshima yanayokubalika kiofisi ndani ya serikali ya Tanzania kwa wanachuo wote ni **LAZIMA**, wakiwa ndani au nje ya chuo. Suruali za kubana, nguo fupi na mavazi yoyote yanayoacha wazi sehemu kubwa za viungo vya mwili kama kifua, tumbo, kitovu, mgongo, makalio n.k haziruhusiwi kabisa chuoni.
9. Wizi, ulevi, ugomvi, kutukana na tabia zingine zote zilizo kinyume na Kanuni na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hazikubaliki.
10. Mwanachuo atapaswa kuvaa kitambulisho awapo chuoni na nje ya chuo.
11. Mwanachuo atashiriki kikamilifu katika kuweka mazingira ya chuo kuwa safi.
12. Ili kujenga na kuimarisha afya za wanachuo, wanachuo wote watalazimika kushiriki kikamilifu katika burudani na michezo wawapo chuoni.
13. Fomu ya mkataba iliyoambatanishwa ijazwe na mwanachuo na mzazi/mlezi/mfadhili kisha isainiwe na kukabidhiwa chuoni wakati wa usajili pindi mwanafunzi anaripoti chuoni. Aidha, utatambulika kama mwanachuo mara baada ya kukamilisha usajili.
14. **Andika jina lako (jina la mwanafunzi) kama lilivyo kwenye vyeti vyako unapofanya malipo Benki na uje na slip ya malipo chuoni wakati wa kuripoti.**
15. Usifanye malipo yoyote kama hujaelewa kwani ukikosea kulipa fedha hazitarudishwa.

**NB:** Endapo utahitaji ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na Mkuu wa Chuo, S.L.P 6, Mafinga. Au piga simu Namba. 0769493600/0767257744 **siku za kazi tu kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.**

**KARIBU CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA**

**KIDUBYA B. KULAMIWA**
**MKUU WA CHUO**

PRINCIPAL
COMMUNITY DEVELOPMENT
TRAINING INSTITUTE
RUNGEMBA

**MKATABA**
**CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUNGEMBA**
**KUKUBALI KUTEKELEZA MASHARTI YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA ASTASHAHADA YA MAENDELEO YA JAMII NA UPANGAJI NA USIMAMIZI WA MIRADI MWAKA 2026/2027**

Mimi……………………………………………………………………………

(Jina kamili la mwanafunzi kwa herufi kubwa)

Nimepokea taarifa ya kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya taaluma ya Maendeleo ya jamii ngazi ya Astashahada/Stashahada katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba.

Kwa hati hii naahidi kwamba nitatekeleza masharti yote niliyopewa katika barua ya kuchaguliwa kujiunga na Mafunzo hayo pamoja na kanuni nitakazopewa chuoni.

JINA LA MWANACHUO…………………………………………………………..

SAINI YA MWANACHUO ……………………………..TAREHE…………….

JINA LA MZAZI/MLEZI …………………………………………………………

SAINI YA MZAZI/MLEZI ………………..……………..TAREHE…………….

NB: Fomu hii ya mkataba irejeshwe chuoni wakati wa usajili

**RUNGEMBA COMMUNITY DEVELOPMENT TRAINING INSTITUTE**

**FEE STRUCTURE FOR BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN COMMUNITY DEVELOPMENT AND PROJECT PLANNING (NTA LEVEL 4) -2026/2027**

**A: PAYABLES AS PER SEMESTER (MWAKA WA KWANZA)**

| ITEM | SEMESTER I | SEMESTER II | MODE OF PAYMENT |
|---|---|---|---|
| Tuition Fee **(Ada ya mafunzo)** | 300,000/= | 300,000/= | Obtain **Control number** from Institute Accountant |
| Registration Fee **(Ada ya usajili)** | 15,000/= | - | Obtain **Control number** from Institute Accountant |
| Accommodation fee (Boarding and Lodging when available) **(Ada ya bweni)** | 100,000/= | 100,000/= | Obtain **Control number** from Institute Accountant |
| Identity card fee **(Ada ya kitambulisho)** | 10,000/= | - | Obtain **Control number** from Institute Accountant |
| Wear and Tear **(Fedha ya uchakavu)** | 10,000/= | - | Obtain **Control number** from Institute Accountant |
| Medical Contribution (NHIF) **(Fedha ya bima ya afya)** | 50,400/= | - | Student will obtain account of NHIF once arrived at the institute (Mwanachuo atapewa akaunti ya kulipia akifika chuoni) |
| First Aid (non refundable) **(Fedha ya huduma ya kwanza)** | 10,000/= | - | Obtain **Control number** from Institute Accountant |
| NACTVET Quality Assurance Fee (Ada ya uhakiki na baraza la vyuo NACTVET) | 20,000/= | - | Institute A/C No. 60202300255 NMB Jina la akaunti: **Rungemba Economic Activities** |
| Examination Fee **(Ada ya mitihani)** | 15,000/= | 15000/= | Obtain **Control number** from Institute Accountant |
| Certification (Certificates & transcript **(malipo ya cheti na slip ya matokeo)** | | 15,000/= | Obtain **Control number** from Institute Accountant |
| | **530,400/=** | **430,000/=** | |

**B: MODE OF PAYMENT (NAMNA YA ULIPAJI)**

| ITEM | AMOUNT | MODE OF PAYMENT |
|---|---|---|
| Contribution to Student Organization (CDSO) **(Mchango wa Umoja wa Serikali ya Wanachuo)** | 10,000/= | A/C No. **01065308** MUCOBA BANK, Account name: CDISO RUNGEMBA CDTI MAFINGA |
| T-shirt ya umoja wa wanafunzi | 15,000/= | Atanunua kwenye ofisi ya umoja wa wanafunzi CDISO |

**C: (POCKET MONEY) MAKADRIO YA MATUMIZI BINAFSI KWA MWANACHUO**

| ITEM | AMOUNT |
|---|---|
| Meals (Chakula) | 850,000 (kwa mwaka) |
| Field allowance (Gharama za mafunzo kwa vitendo) NB: *Pata ufafanuzi chuoni* | 300,000 (kwa mwaka) |
| Books and stationery (gharama za stationari) | 150,000 (kwa mwaka) |



PRINCIPAL
COMMUNITY DEVELOPMENT
TRAINING INSTITUTE
RUNGEMBA